K.C.S.C. 003

GATUZI NDOGO YA KISII YA KATI
K.C.P.E DARASA LA NANE
MUHULA WA TATU 2014

KISWAHILI

Muda: Saa 1 Dakika 40

SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lionyeshe katika **KARATASI YA MA JIBU** na wala sio katika kijitabu cha maswali.

JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu: -

   NAMBARI YAKO YA MTIHANI

   JINA LAKO

   JINA LA SHULE YAKO
6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye nambari zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani nambari ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu
9. Kwa kila swali 1-50 umeepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

Mfano:

Katika kijitabu cha maswali:

Kutoka swali 16 - 30 chagua jibu sahihi.

17. Konsonati za lugha ya kiswahili ni ngapi?

    A. 26

    B. 25

    C. 21

    D. 30

    Jibu sahihi ni B.

7. [A] [B] [C] [D] **17.** [A] ~~[B]~~ [C] [D] **27.** [A] [B] [C] [D] **37.** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 17, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

FUNGUA KURASA

Karatasi hii ina maswali 50 iliyopigwa chapa.

_____1_____ ya elimu yanajitokeza ___2___ upana wilayani. _____3___ yanatokea kuwa kama mojawapo ___4___ _____5_____ yaliyopowea umuhimu na wenye vyeo ___6___ nchi ya Adili. Tunafahamishwa kuwa Busara alielimishwa katika shule za misheni _____7___ alihitimu ___8 ___ kufika darasa la nane. Lengo lake ni _____9_____ ukasisi baada ya kukamilisha masomo ya shule ya upili. Yeye ni _____10_____ watu wachache wanaoenzi gange hiyo.

	A.	B.	C.	D.
1.	Lengo	Kusudi	Maudhui	Shabaha
2.	na	kwa	katika	kwenye
3.	Aghalabu	Isipokuwa	Maadamu	Mradi
4.	wa	za	kwa	ya
5.	maswali	masuala	i natatizo	maendeleo
6.	kwa	kutoka	k wenye	katika
7.	ambako	ambamo	at nbapo	kwenye
8.	juu ya	badala ya	ba ada ya	kabla ya
9.	kusoma	kusomesha	kus omewa	kusomea
10.	miongoni mwa	mighairi ya	bigh airi ya	kwa ajili

Mtu mmoja alifariki ___11__ juzi huku ___12___ akiachwa na __ _13___ mabaya _____14_____ ajali ___15_____.

	A	B	C	D
11.	papo huko	papo hapo	papo pa po	papo hapa
12.	nyingine	wengine	mwingi ie	kwingine
13.	majaruhi	mabaka	machozi	majeraha
14.	kufuatia	kufuata	kwa	kwa sababu
15.	baya	mbaya	mibaya	mabaya

Kutoka swali la 16 - 30, jibu kulingana na maagizo.

16. **Kanusha:** Angalianguka angaliumia
A. Hangeanguka hangeumia
B. Asingeanguka asingeumia
C. Asingalianguka asingeumia
D. Asingalianguka asingaliumia

17. Ni kundi lipi haliambatani?
A. Mundu, Susu, Toroli, Makoongo
B. Kibanda, Msonge, Baiti, Ikulu
C. Jambia, Gumegume, Kombeo, Mzinga
D. Kikandio, Uyoka, pambajio, Koleo

18. Andika tarakimu hii kwa maneno 999696
A. Laki tisa elfu tisa mia sita tisini na sita
B. Laki tisa elfu tisini na tisa mia sita tisini na sita
C. Laki sita elfu tisini na tisa mia sita tisini na sita
D. Laki tisa elfu tisini na tisa mia tisa sitini na sita

19. Chagua kundi la nomino dhahania.
A. Maji, uji, maziwa
B. Kiti, uteo, nyua
C. Jozi, mkungu, halaiki
D. Upendo, zuri, wema

20. Ainisha maneno yaliyopigiwa kistari
Uandishi wake ulimpendeza mwanafunzi huyo.
A. Kivumishi, kiwakilishi
B. Kimilikishi, kiambishi
C. Kivumishi, kionyeshi
D. Kiashiria, kiunganishi

21. Nyambua kitenzi "Lia" katika kauli ya kutendesha
A. Liza
B. Laza
C. Lisha
D. Lilia

22. Maana ya nahau chimba mtu ni
A. Fukia maiti
B. Fitini mtu
C. Fukuza mtu
D. Danganya mtu

23. Ni sentensi ipi yenye kielezi cha wakati?
A. Sherehe itakuwa mesini
B. Yeye hutuzwa mara nyingi
C. Nitaenda ughaibuni mwakani
D. Bi tausi amevaa kiungwana

24. Ni methali ipi isiyowiana na nyingine?
A. Mtu ni watu
B. Upweke ni uvundo
C. Kofi hazilii ila kwa viganja viwili
D. Maji yakijaa hupwa

25. Nomino Mbwa ina sauti ngapi?
A. Mbili
B. Tatu
C. Nne
D. Moja

26. Ukubwa wa wingi wa sentensi hii ni, Nguo hiyo inapendeza mtoto huyu. _____
A. Maguo hayo hanayapendeza matoto haya
B. Nguo hizo zinawapendeza watoto hao
C. Viguo hivyo vinavipendeza vitoto hivyo
D. Manguo hayo yanapendeza matoto haya

27. Papa ni kwa kinengwe,nyani ni kwa _____
A. Tumbili
B. Kigunge
C. Kinyani
D. Kunyaunyau

28. Hekima alihamia nchi nyingine na kufanya makao yake humo. Yeye ni
A. Mlowezi
B. Mtalii
C. Mtoro
D. Mkimbizi

29. "Kwa" imetumikaje katika sentensi hii Sherehe hiyo ilihudhuriwa na wazee kwa vijana.
A. Matumizi
B. Kimikilishi
C. Mahali
D. Pamoja naa

30. Tambua kihisishi cha kudhihirisha kushtuka
A. Taib!
B. Afanalek!
C. Po!
D. Pukachaka!

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali kutoka 31 hadi 40.

Tabu alizaliwa katika familia iliyogubikwa na uchochole kupindukia. Kupata chakula angaa mara moja kwa siku ilikuwa ndoto isiyotabirika kwao. Walitegemea chakula cha msaada kutoka kwa serikali na wasamaria wema. Maisha yao yalikuwa yamesakamwa na wingu jeusi.

Si hayo tu, msanii Tabu alipoteza mamake akiwa na umri mbichi wa miaka 10 pekee, akabaki mikononi mwa babake aliyekuwa amezama katika lindi la ulevi chakari. Maisha yalimwia magumu hadi akawa anaishi na kusoma kutumia kudura za Mwenyezi Mungu tu!

Mnamo mwaka wa 2005, babake aliaga dunia baada ya kuugua kwa muda mfupi, akabaki yatima. Miaka minne baadaye, kama kuongeza msumari moto katika donda ndugu, dadake wa kipekee pia aliaga dunia kwa njia shani naye kaka yake wa toka nitoke, akashikwa na wazimu. Kimako kweli!

"Kuaga dunia kwa wazazi na dadangu, na pia kakangu kuingiwa na kichaa kulijaza huzuni na simanzi fuadini mwangu. Watu wa nasaba yangu na majirani walianza kunitega wakadai nimetoka katika familia ya laana. Hakika, niliteseka sana". Asema.

Tabu asema kwamba, alipofanya mtihani wa KCPE mwaka wa 2007 na kufuzu vyema, alijiunga na shule ya upili ya Busara, kaunti ya Kware. Kwa minajili ya ukosefu wa fedha za kulipia karo, alibahatika kupata mdhamini, John Mwema hadi akahitimisha kidato cha nne.

Mwaka huo huo, Tabu alifadhiliwa na wahisani mbalimbali kurekodi albamu yake ya kwanza na ikavuma mithili ya wimbi la bahari.

"Kuvuma kwa wimbo huo kulinisukuma nijitose katika mkurumbuto wa kuwania taji la 'Groove Awards', lakini sikuweza kufua dafu wakati huo maana nilikabiliwa na upinzani mkali". Asema msanii huyu mcheshi.

Hata hivyo, kana kwamba mikururo ya mikosi na kisirani ilikuwa bado inamwandama, msanii huyu alihusika katika ajali ya barabarani na akapoteza jicho moja. Alishindwa ni wapi alimkosea Mungu ili azidi kukumbwa na masaibu hayo.

Waama, Mungu hamtupi mja wake. Alipata afueni mwezi uliopita wakati alipoanza kupata mialiko ya kutumbuiza katika maeneo mengi barani mwetu.

31. Ni kweli kusema kuwa;
A. Tabu alipata chakula kwa urahisi
B. Tabu aliishi maisha ya ulalaheri
C. Familia ya Tabu ilikuwa fukara
D. Familia ya Tabu ilipeana chakula cha msaada

32. Mwandishi anasema yafuatayo yalizidisha maji unga isipokuwa _____
A. kakaye kuwa punguani
B. mauti ya wavyele wake
C. kifo cha dadaye
D. kupewa vyakula vya msaada

33. Fuadi ni kisawe cha
A. Roho
B. Mtima
C. Buki
D. Akili

34. Kulingana na kifungu _____
A. Tabu alifadhiliwa na mhisani mmoja tu.
B. Mwandishi hakufuzu katika mtihani wa K.C.P.E
C. Ufadhili wa wahisani mbalimbali ulimfaa
D. Licha ya upinzani mkali Tabu alifuzu kuwania taji.

35. Ni methali ipi inayowiana na "Mungu hamtupi mja wake"
A. Mungu si athumani
B. Liandikwalo halifutiki
C. Bidii haiondoi kudura
D. Wino wa Mungu haufutiki

36. Tabu alishangaa iwapo alimkosea Mola kwa sababu _____
A. Alipata ajali na kupoteza jicho
B. Hali ya kuachwa yatima
C. Kakaye kupata ugonjwa wa kichaa
D. Mikosi ilimwandama mmoja baada ya mwingine

37. Mkururo wa mikosi kama ilivyotumiwa katika kifungu ni
A. mikosi michache
B. mikosi ainati
C. mikosi mibaya
D. mikosi kadhaa

38. Kinyume cha 'laani' ni nini kulinana na kifungu
A. Kashifu
B. Sifu
C. Bariki
D. Thamini

39. Mwandishi anaweza kusema amefaulu maishani kwa kuwa _____
A. hajapata mikosi hivi karibuni
B. amefadhiliwa na wahisani wengi
C. alipoteza jicho moja katika ajali
D. amekuwa mashuhuri katika usanii

40. Kichwa kifaacho zaidi makala haya ni ___
A. Ukiona vyaelea vimeundwa
B. Atangaye sana najua hujua
C. Bidii ya mja haiondoi kudura
D. Kila mwamba ngoma huivuta kwake

Soma kifuungu kifatacho kisha ujibu maswali 41 hadi 50

Katika utamaduni wa jamii yoyote ya Kiafrika, kulikuwa na mihimili muhimu ambayo ilihakikisha kuwa tamaduni hizo zimedumishwa na kulindwa dhidi ya matishio yoyote yale yalonekana kuhatarisha uwepo wake.

Kwa mantiki hiyo, udumishaji wa tamaduni hizo uliwianishwa na mihimili muhimu kama wazee, mandhari fulani nyimbo, ngano, mavazi, mitindo ya kimaisha, vyakula, aina ya makazi kati ya mengine.

Na ilivyokuwa katika jamii hizo, uchakachuzi wowote wa mmoja wa mihimili hiyo, ulikuwa na athari kubwa sana kwa uthabiti, upasishaji wa tamaduni husika kutoka kizazi kimoja hadi kingine pamoja na mustakabali wake kwa jumla.

Narejelea haya kutokana na kilio ambacho kimesikika kutoka kwa wazee wa jamii ya Wamijikenda, wakilalamika kuvamiwa na kuharibiwa kwa misitu ya kiasili ya Kaya na wajenzi, huku kilio chao kwa mamlaka husika kikionekana kutozingatiwa na yeyote.

Kwa urejeleo mfupi, misitu hiyo imekuwa na umuhimu mkubwa katika udumishaji wa utamaduni wa Wamijikenda, ambako imeipa utambuzi kama mojawapo ya jamii chache ambazo zimeendelea kufaharikia utamaduni wake, licha ya mienendo ya kisasa ambayo imekuwa ikihatarisha uwepo wa tamaduni za jamii nyingine nchini.

Mojawapo ya hafla muhimu ambazo zimekuwa zikihusishwa na misitu hiyo ni maombi ya kiasili ya jamii hiyo yanayoendeshwa na wazee maalum ambao huwa wanaheshimika sana.

Wazee hao huwa na umuhimu mkubwa sana kwa jamii hiyo, kiasi kwamba si mara moja tumewaona wanasiasa wenye hadhi nchini wakiwaendea kwa utakaso, kabla ya kutawazwa rasmi kama wazee wa jamii ya Wamijikenda.

Mmoja wa wanasiasa ambao waliwahi kuonyesha umuhimu wa uzingatiaji wa tamaduni ni aliyekuwa waziri wa serikali za mitaa marehemu Bw Mwendapole, ambaye alitokea kuwa mzingatiaji na mlinzi mkuu wa tamaduni za jamii yake. Wengine ambao wamewahi kwenda kupata baraka za wazee hao ni pamoja na Busara, Fadhili na Akilipevu.

Kuu linalojitokeza hapa ni kuwa viongozi hao wamekuwa mfano mwema wa wazalendo wanaotambua kuwa mojawapo ya mhimili mkuu wa Uafrika ni uzingatiaji wa tamaduni zilizomo.

Lakini yasikitisha kuwa wajenzi wanaponyakua hao ya kibinafsi na wazee hao kupasa sauti zao wakitaka msaada wa wanasiasa ambao kwa njia moja ama nyingine wamenufaika moja kwa moja kutokana nayo; hakuna anayeonekana kuzingatia kilio chao.

Ni picha mbaya kwa serikali na taasisi zinazohusika katika udumishaji wa turathi zetu za kitaifa kuwa uharibifu wa maeneo huhimu kama hayo unaweza kuwa ukiendelea, huku kukikosa uingiliaji wa aina yoyote ili kuyanusuru.

Ukweli uliopo ni kuwa maeneo mengi ya jadi ambayo yalihusishwa na tamaduni muhimu za kizamani za jamii mbalimbali yanaendelea kutelekezwa na kuangaliwa tu; yanapoendelea kuathirika.

Baadhi ya maeneo hayo ni pamoja na misitu muhumu ya kitamaduni kama ule wa Mlima Kenya na Aberdare, ambao ulitumiwa na wapiganaji wa Mau Mau katika vita vya ukombozi wa taifa hili kutoka kwa wakoloni.

Uharibifu wa misitu hiyo unahatarisha mustakabali wa historia ya Mau Mau. Aghalabu kuna ngome na mashimo mengine muhimu yaliyotumiwa na wapiganaji hao, ambayo kando na kutopata utambuzi, kuna hatari yake kusambaratika bila hata historia yake kunakiliwa.

Ikumbukwe kuwa mwoano wa historia ya nchi na utamaduni wake ni muhimu sana, na ndiyo huwa mihimili ya mustakabali wake, hasa kunapoibuka tishio za mwingilio wa tamaduni za kigeni.

41. Kulingana na aya ya kwanza ni kweli kusema _____
A. tamaduni mbalimbali zilifutiliwa mbali baada ya muda.
B. hakukuwa na tishio zozote zilizopinga tamaduni.
C. katika bara la Afrika tamaduni zilidunishwa kwa kiasi kikubwa
D. kulikuwa na udumishaji wa tamaduni dhidi ya tishio mbalimbali.

42. Katika bara la Afrika kudumisha kwa tamaduni kuliwianishwa na mihimili hii yote ila ____
A. hadithi
B. elimu
C. makazi
D. vyakula

43. Wanajamii wanalalamikia nini kulingana na kifungu? _____
A. Kuharibiwa kwa misitu
B. Kuharibiwa kwa misitu asili
C. Kuvamiwa kwa wanyama pori
D. Mamlaka duni katika jamii hizo

44. Kulingana na kifungu misitu ina umuhimu upi? _____
A. Kudunisha utamaduni
B. Ni chemichemi za maji
C. Ni vianzo vya mito mbalimbali
D. Kuboresha tamaduni

45. Kati ya watu waliopigania utamaduni udumishwe si pamoja na _____
A. Hekima
B. Fadhili
C. Mwendapole
D. Busala

46. Nomino 'Mzalendo' kama ilivyotumiwa kwenye makala ina maana _____
A. anayepeleza jambo fulani
B. raia katika taifa fulani
C. mwenyeji wa pahali
D. aipendaye nchi yake

47. Kwanini wazee maalum katika jamii inayozungumziwa huheshimika?
A. Huongoza maombi ya kiasili kanisani
B. Wanasiasa wenye hadhi huwapa hela za miundomsingi
C. Huongoza sala za kiasili katima misitu
D. Huombea jamii hiyo faraghani

48. Usemi huu una maana gani kama ulivyotumika katika taarifa? "yanaendelea kutelekezwa na kuangaliwa tu; yanapoendelea kuathirika"
A. Maeneno mengi ya kitamaduni yamepewa hadhi ya juu
B. Maeneo yaliyohusishwa na tamaduni muhimu yamepuuzwa
C. Jamii mbalimbali zimeteketeza misitu na turathi
D. Milima na misitu mbalimbali inatumiwa kama vivutio vya watalii

49. Uharibifu wa misitu muhimu ya kitamaduni umesababisha haya yote isipokuwa ___
A. ongezeko la watalii nchini
B. kuhatarisha kwa historia za waliopigania uhuru
C. kusambaratika kwa ngome za wapiganaji wa uhuru
D. kuzika historia muhimu katika kaburi la sahau

50. Ni methali ipi ifaayo makala uliyoyasoma?
A. Mchezea tope humrukia
B. Jungu kuu halikosi ukoko
C. Mwacha mila ni mtumwa
D. Meno ya mbwa hayaumani